

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



Mtaa wa Bagara Miomboni,  
S.L.P. 386,  
27103 MANYARA,  
Barua Pepe: [rbcmanyara@pccb.go.tz](mailto:rbcmanyara@pccb.go.tz).  
**TANZANIA.**  
[www.pccb.go.tz](http://www.pccb.go.tz)

**MANYARA – JANUARI 04, 2020**

**TUNAWATAKA WALIOKOPA MATREKTA WAREJESHE**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoani Manyara imepewa jukumu la kuhakikisha kuwa wakulima waliokopa mikopo ya Matrecta kutoka Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC) inarejeshwa na zoezi la urejeshwaji linaendelea mkoani Manyara.

Serikali kupitia shirika lake la maendeleo ya Taifa (NDC) mnamo mwaka 2018 iliwakopesha wakulima Matrekta katika mipango ya Serikali ya kuhakikisha wakulima wanaondokana na kilimo cha jembe la mkono.

Katika Mkoa wa Manyara wakulima walihamasishwa na wakakopa zana hizo za kilimo ambapo thamani ya Matrekta yaliyokopeshwa Mkoani Manyara ni zaidi ya shilingi bilioni saba (Sh. 7,565,215,000/=). Mikopo hii ilichukuliwa na wakulima katika Wilaya za Babati, Hanang, Simanjiro, Mbulu na Kiteto.

Tunawapongeza wakulima wa Wilaya za Babati na Mbulu waliochukua mikopo hiyo ambapo wengi wao wameonyesha ushirikiano mzuri kwa maafisa wetu, kwani wameendelea kulipa madeni ambayo wamekuwa wakidaiwa kwa mujibu wa mikataba yao.

Aidha katika wilaya ya Kiteto kumejitokeza walaghai (Bush Lawyers) ambao tumesikia wanahamasisha wakulima kukwepa kurejesha mikopo hiyo kwa maelezo kuwa mikopo ya Serikali huwa hairejeshwi. Tunapenda kuujulisha umma wa wanaManyara kwamba, uhamasishaji huo ni haramu na kwamba wakulima waliochukua mikopo wawapuuzze na waendeleo kurejesha. Aidha tumeanzisha uchunguzi kwa wanaohusika na ulaghai huo na watakaobainika watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria bila kujali hadhi zao katika jamii.

Rai yetu kwa wawakilishi wa wananchi wakiwemo Madiwani na Wabunge ni kwamba tushirikiane kuwahamasisha wananchi waliochukua mikopo hiyo katika maeneo yao, wairejeshe ili wananchi wengi zaidi waweze kukopeshwa Matrekta kutokana na fedha hizo. Nia ya Serikali ni kuwawezesha wakulima wengi zaidi kufanya kilimo cha kisasa na chenye tija.

**Imetolewa na:**

**HOLLE MAKUNGU  
MKUU WA TAKUKURU (M)  
MANYARA**